**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA


**Mtaa wa Mahenge,**
**S. L. P. 926,**
**57101 RUVUMA.**
**Barua pepe:**
**rbcruvuma@pccb.go.tz**
**TANZANIA**
**Wavuti : http://www.pccb.go.tz**


**RUVUMA – APRIL 28, 2022**

## MIRADI YA ZAIDI YA BILIONI TANO YAKAGULIWA RUVUMA.

**Ndugu wanahabari.**
Tumekutana tena katika ofisi yetu ya TAKUKURU Mkoa wa Ruvuma ili tuweze kuuhabarisha umma kuhusu utendaji kazi wa ofisi yetu kwa kipindi cha miezi mitatu kuanzia mwezi wa Januari 2022 hadi Machi 2022.

### UCHUNGUZI

Katika kipindi cha Januari hadi Machi 2022, imeweza kutekeleza majukumu yake ya uchunguzi na kufanikiwa kupokea jumla ya taarifa mpya **45** za malalamiko mbalimbali. Kati ya taarifa hizo, malaamiko **33** yalikuwa na viashiria vya rushwa na taarifa 12 hazikuhusu Rushwa. Taarifa 33 zilizohusu Rushwa, zilifanyiwa uchunguzi wa awali ambapo taarifa 1 imefungwa kwa kukosa ushahidi, taarifa 25 uchunguzi wake bado unaendelea na taarifa 7 uchunguzi wake umekamilika. Aidha **taarifa 12 ambazo hazikuhusu rushwa**, walalamikaji 10 walishauriwa kupata msaada kwenye taasisi husika na taarifa 2 zimehamishiwa katika idara nyingine.

### MASHTAKA
Kwa upande wa Mashtaka katika kipindi hiki tuliweza kufungu **kesi moja** katika mahakama ya wilaya ya Mbinga na hivyo kufanya jumla ya **kesi 6** ziliendeshwa mahakamani.

## UZUIAJI RUSHWA

Katika kipindi cha Januari hadi Machi 2022 kwa upande wa Uzuiaji Rushwa, TAKUKURU mkoa wa Ruvuma imefanikiwa kufanya chambuzi za mfumo **sita (6), kuhusu utendaji kazi wa wakala wa huduma ya manunuzi ya serikali (GPSA) na wakala wa huduma wa ufundi na umeme (TEMESA)** katika Halmashauri ya Manisapaa ya Songea, **viashiria vya rushwa ya ngono katika sekta ya elimu** katika Halmashauri za Wilaya ya Songea, Tunduru na Namtumbo. Kufutia chambuzi hizo yalibainika mapunufu mbali mbali yakiwemo yenye viashiria vya rushwa, hivyo TAKUKURU mkoa wa Ruvuma ilifanya vikao vya warsha na wadau ili kujadili matokeo ya chambuzi zilizofanyika ikiwa ni pamoja na kuweka malengo ya utekelezaji ili kutafuta ufumbuzi wa changamoto zilizobainika.

## UFUATILIAJI WA MATUMIZI YA FEDHA ZA MPANGO WA MAENDELEO KWA USTAWI WA TAIFA NA MAPAMBANO DHIDI YA UVIKO 19

Katika kipindi hiki cha miezi mitatu TAKUKURU Mkoa wa Ruvuma imefanya ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo yenye thamani ya jumla ya shilingi **Bilioni tano milioni mia nne themanini na saba, laki sita thelathini na sita, mia moja tisini na nane na senti tisini na mbili** (**5,487,636,198.92),** ikiwemo kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo kupitia **Mpango wa maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya Uviko-19** yenye thamani ya jumla ya shilingi **milioni mia moja na sitini (160,000,000/=).** Hii ni miradi ya ujenzi wa vyumba 8 vya madarasa katika shule za sekondari Ruhuwiko, Mbambi, Ruanda pamoja na Mbinga Girls zilzoko katika Wilaya ya Mbinga ambayo mpaka wakati wa ukaguzi wake ilikuwa imekamilika. Ikumbukwe kuwa maendeleo ya nchi huletwa na wananchi wenyewe, ambao ni wewe na mimi.

## ELIMU KWA UMMA

TAKUKURU mkoa wa Ruvuma katika kipindi cha miezi mitatu imeendelea na jukumu la kuelimisha umma kwa kuyafikia makundi mbalimbali ya jamii lengo likiwa ni kuendelea kuwajengea uelewa wa madhara ya rushwa, ili waweze kushiriki katika mapambano dhidi ya

rushwa. Tumefanya Semina 33, klabu za wapinga rushwa 91 za shule za msingi na sekondari ziliimarishwa, mikutano ya hadhara 27 ilifanyika, Makala 8 ziliandaliwa, vipindi viwili (2) vya redio vilirushwa pamoja na taarifa kwa Umma moja ilitolewa.

## TAKUKURU INAYOTEMBEA

TAKUKURU Mkoa wa Ruvuma iliendelea na zoezi la kutembelea wananchi katika maeneo yao kwa lengo la kusikiliza kero za rushwa. Katika kipindi cha miezi mitatu tumeweza kutembelea maeneo ya baadhi ya vijiji huko wilayani na baadhi ya vitongoji vya hapa Manispaa na kufanikiwa kupokea kero mbalimbali za rushwa na makosa mengine. Kwa zile taarifa ambazo hazihusianani na rushwa tumekuwa tukiziwasilisha kwenye Mamlaka husika ili ziweze kufanyiwa kazi na wananchi kupewa mrejesho.

## UTEKELEZAJI WA USHIRIKIANO WA TAKUKURU NA SKAUTI - TAKUSKA

TAKUKURU Mkoa wa Ruvuma kwa kushirikiana na vijana wa Skauti kwa pamoja imeendelea kutoa elimu ya mapambano dhidi ya rushwa ikiwa na lengo la kujenga uadilifu, uwajibikaji na uzalendo kwa vijana walioko katika shule za msingi na sekondari ambapo TAKUKURU iliweza kushiriki katika shughuli za uhamishaji wa vijana kujiunga na Skauti kwa Wilaya za Mbinga na Nyasa.

## MAADHIMISHO YA SIKU YA WANAWAKE DUNIANI.

TAKUKURU inatambua umuhimu wa siku ya wanawake Duniani na hivyo Watumishi wa TAKUKURU waliopo katika mkoa wa RUVUMA walijumuika pamoja na wanawake wa mkoa huu katika kuadhimisha siku hii ya Kimataifa ya wanawake Duniani yaani machi 8, 2022. Maadhimisho hayo yalifanyika kimkoa katika halmashauri ya wilaya ya Madaba, pamoja na kauli mbiu ya siku hiyo Kitaifa iliyosema "**kizazi cha haki na usawa kwa maendeleo endelevu**" TAKUKURU ilibeba ujumbe wa "Vunja **UKIMYA KATAA RUSHWA YA NGONO**" na kuwaelimisha baadhi ya wanawake walioambatanao juu ya madhara ya rushwa ya ngono hasa kwa wanafunzi wa kike.

## MAADHIMISHO YA WIKI YA SHERIA NCHINI

TAKUKURU kama mdau mkubwa wa masuala ya sheria ilishiriki pia maadhimisho ya wiki ya sheria nchini yaliyofanyika katika viwanja vya Manispaa ya Songea na kauli mbiu ilisema "mapinduzi ya nne ya wiwanda safari ya maboresho kuelekea mahakama Mtandao". Pamoja na mambo mengine tulifanikiwa kuwa na banda la maonesho tukitoa elimu ya mapambano dhidi ya Rushwa na namna TAKUKURU inavyo fanya kazi kwa kushirikiana na Mahakama.

## MATARAJIO YETU KWA KIPINDI CHA APRILI – JUNI 2022.

Katika kipindi cha miezi mitatu ijayo tumejipanga kufanya mambo yafuatayo: -

1. Kuendelea kuelimisha wananchi juu ya rushwa na madhara yake katika usimamizi wa miradi ya maendeleo lengo ni kuwawezesha wananchi kupata uelewa na kuweza kusimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa karibu na weledi wa hali ya juu.

2. Tutaendelea kufanya kazi za uzuiaji rushwa kwa lengo la kubaini mianya ya rushwa katika maeneo mbalimbali zikiwemo taasisi za Umma na Binafsi na kushauri namna bora ya kuiziba mianya hiyo. Pia natoa wito kwa wakurugenzi wa halmashauri zote za mkoa wa Ruvuma kuendelea kutoa ushirikiano wa hali ya juu wakati wote wa kutekeleza miradi ya mpango wa maendeleo kwa ustawi wa taifa na mapambano dhidi ya uviko-19 katika tawala za mikoa na mamlaka za serikali za mitaa pindi utakapo hitajika.

3. Tutaendelea kufanya uchunguzi na kuwachukulia hatua wale wote watakao kutwa na tuhuma za vitendo vya rushwa ikiwa ni pamoja na kuwafikisha Mahakamani.

4. TAKUKURU kwa kushirikiana na vijana wa Skauti tutaendelea kutoa elimu ya mapambano dhidi ya rushwa ikiwa na lengo la kujenga uadilifu, uwajibikaji na uzalendo kwa vijana walioko katika shule za msingi, sekondari, vyuo vya kati na vyuo vikuu.

Baada ya kusema hayo nipende kuwapongeza wananchi wote wa mkoa wa Ruvuma kwa jinsi wanavyoendelea kushirikiana na TAKUKURU katika kufichua vitendo vya rushwa. Ninawasihi kuendelea kushirikiana na TAKUKURU kwa kutoa taarifa za vitendo vya rushwa nasi tunaahidi kuzifanyia kazi taarifa tutakazo zipokea kwa wakati.

**Imetolewa na:**

HAMZA MWENDA
**MKUU WA TAKUKURU MKOA WA RUVUMA**
Nambari ya simu: SIMU BURE 113
MKUU WA TAKUKURU (M) 0738 150 190
NAIBU MKUU WA TAKUKURU (M) 0738 150 191